https://dspace.org/

# Fasili zilizofichamana katika maneno Shenzi (Zenj) na Nyoko

**Mohamed, Karama**

**2022-12**
Gombo La Isimu Tumi Ni Kufuwata Sat I Za Majagina Wa Isimu
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/506

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

DKT. MOHAMED KARAMA, UNIVERSITY OF KABIANGA

# Fasili zilizofichamana katika maneno Shenzi (Zenj) na Nyoko

**Viḏahizo:** 1) Kwa maneno ya Shekhe langu, Marehemu Sheikh Sheeali Omar Mbarak, alinambiya siku moja, "hizo elimu mbaya nazisomwe ili watʰu wapate kuzijuwa". Katika makala haya tuṯaṯowa maṯushi ambayo kiḏasturi ni mwiko kuyaṯamka hadharani lakini imetubidi tuweke wazi mambo fulani ili wanaṯaalimu, nikiwamo, tuweze kufaidika. 2) Munamo 2011, tulipokuwa tukifanya tʰafiṯi zetu RISSEA, tuliwahi kumwanḏikiya Profesa wangu, Kimani Njogu, na Tume ya Ushikamano na Uṯangamano wa Kiṯaifa (NCIC) kuhusu neno hili 'shenzi' linavotumika kwenye moja ya kampeni za 'kuwasṯaarabisha waKenya'!

Makala haya mafupi yana madhumuni ya kuṯowa ufunuzi, ingawa mchache, kuhusu maneno hayo mawili: shenzi na nyoko yaliyohifadhiwa kwenye maṯushi, hivi leo, lakini yenye maana kʰuu katika mapisi ya na uṯamaduni wa wenyeji wa pwaa hizi za Afrika Mashariki. Uchunguzi wetu ulikuwa ni wa kisinkroniya kwa kutumiya mawanda ya Fonolojiya. Zaidi, uchanganuzi wetu ulikuwa wa mapitiyo ya kazi zilizoanḏikwa kuhusu nyusuli za maneno haya na mukṯadha wa matumizi. Ufafanuzi wa shenzi uṯahusu usuli wake, matumizi yake, na ulinganifu wake katika mapisi ya waSwahili na uSwahilini. Ama, nyoko tuṯalenga kwenye usuli na matumizi yake katika uṯamaduni wa waSwahili. Lengo kʰuu ni kubaḏilisha kasumba—zilizokuja kwa juu—zilizofungamanishwa na maneno hayo ambayo asili yake ni ṯwahara, chembelecho marehemu Mr. Alwy Saggaf (Mwalimu wetu Tom Mboya Primary School kabla ikiitwa Kongowea School, Mambasa).

## Shenzi

Kulingana na Kamusi ya TUKI (1981) 'shenzi' ni '-enye kutokuwa na ustaarabu, -enye tabia na vitendo visivokubaliyana na nyendo za jamii'. Ukali wa hisiya za mtʰu huonekana wakaṯi wa matumizi ya 'shenzi' katika maongezi ya kikawaida, kwa mfano, kama ilivotumika katika *Nyongo Mkalia Ini* uk. 25, "Huyo mwalimu aliyekufunza ushenzi huo ni nani?" na mukṯadha wa maneno hayo. Na matumizi yake piya hayana mipaka ya umri, ṯabaka, wala jinsiya – yaweza kutumiwa na mtʰu yoyoṯʰe kwa yoyoṯʰe kwa maana hiihii ya kutukana. Kamusi hiyo imeeleza kuwa shenzi ni sifa, ushenzi ni ṯabiya, na mshenzi ni mtʰu mwenye ṯabiya/sifa hiyo.

## Usuli wa neno hili

Katika ṯʰafiṯi zilizofanywa kuhusu neno hili imekisiwa kwamba laṯokana na waandishi wa kiArabu wa Zama za Kati walipokuwa wakiyanḏika maanḏiko yao kuhusu jamii za ulimwengu. Neno lenyewe haswa lililotumiwa ni waṯaalamu hao ni 'zanj/zanji/zinji/zunuj' (Tolmacheva, 1986). Wakaṯi wa uchanganuzi wake, mṯafiṯi huyu aliyeleza kuwa ni jina la kijumuishi linalorejeleya mahali au jamii. Na humo akaeleza kwa kina kuwa 'zanj' linahusu watʰu mahasusi huriya wanaokaa katika upwa wa Afrika Mashariki kanro na sehemu za uSudan, uHabashi na Pembe ya Afrika. Fauka ya hayo, anakʰitʰa kuwa uṯafiṯi wa maanḏiko ya waanḏishi hawa yaonesha waliyanza kulitumiya katika Karne ya 8 na kaṯu

halikumaanisha wala kunasibishwa na rangi ya watʰu wanaozungumziwa. Kwa kutumiya mfano wake, anasema al Istakhri anatumiya neno 'zanj nyeupe' (uk. 111) na kwamba lau zanj ni weusi basi iṯakuwaje nyeusi nyeupe! Wasifu mwengine unaoonesha kuwa 'zanj' ni watʰu wa huku Afrika Mashariki ni kwamba katika maanḏiko ya waanḏishi hawo misamiyaṯi inayoṯolewa mifano ni yenye asili ya kiBantu. Anahiṯimisha basi, yaonekana maana halisi ya neno hilo ni kiArabu; kinyume na inavoarifu nakalape ya kamusi ya TUKI inayolinasibisha neno hili na kiAjemi. Pili, neno hili lilikuwa halina athari za kiurangi ila zilikuja kwa juu athari hizo jambo analolihojiya Shaaban (1978) kwamba athari hizi ziliṯokana na kasumba za ukoloni wa kimagharibi kujaribu kupotosha kuwa waZanji (waSwahili kama tuṯakavokuja kuthibiṯisha baaḏaye) wa Iraq walikuwa watumwa na ilhali sivo. Sibina kuwa kasumba hizi ziko mpaka leo kwani maana moja ya 'mSwahili' ni 'mtu mjanja, mkora' ama kama Dkt. Rotich alivoniarifu kuhusu 'Kipsoiliot' inayomrejeleya mSwahili lakini mukṯadha wake ni huwo wa kasumba potofu.

**Kauli yetu kuhusu usuli huu**

Tʰwaafikiyana na maelezo yao kuhusu neno 'zanj' kuwa ni watʰu au ni mahali lakini Tolmacheva alinakisika wakaṯi alipotaja kuwa kuna majina mengine yanayohusiyana na 'zanj' na mojawapo akasema ni 'waShenzi' (wingi wa m-Shenzi) lakini akaṯahadharisha kuwa neno hili lina athari ya kimwiko/kimatusi (uk. 111-2). Ni wazi kuwa mṯafiṯi huyu alichukuwa maana ya makamusi tajika ya kiSwahili bila ya kwangaliya usuli wake wa kifonolojiya kama alivofanya kuhusu 'zanj'. Sacleux (1939, uk. 602) ametaja kuwa shenzi lina maana ya 'isosṯaarabu' na piya ni 'ardhi/sehemu ya wenyeji wa bara/nyika ya Afrika Mashariki' – miji ilopakana na visiwa va Pemba, Zanzibar. Krapf (1882, uk. 247) alimtaja mShinzi (mShenzi) kuwa mwenyeji wa waShinzi wanaoishi pwani baina ya Mto Pangani na Usambara. Sacleux piya ameuweleza mkoche/mkoma kuwa 'mnazi wa mashenzini' (uk. 562) alipohusisha 'shenzi' katika maana zake mbalimbali. Nrugiyangu Mbarak Abdulkadir piya aliniarifu kuwa huko visiwani Lamu, Kenya piya kuliitwa mashenzini. Sacleux uk. 1038-9, hali kadhalika, alifafanuwa kuwa 'Zanjibar/Zingebar/Zengebar/Zanjibari/' yaṯokana na maneno mawili 'zanji' (mwafrika) na 'bar' (nchi kavu/bara). Na 'zanjifuri' (inayotwonrowa kwenye weusi) ni zaafarani (saffron) rangi yenye wekunru/manjano inayotumika katika uṯabibu au mapishi. Kuṯokana na makamusi haya ya kale, tulopata kuyaona wakaṯi wa uṯafiṯi wetu, hatuna budi kupanuwa au kuiregesha maana ya asili ya shenzi/shinzi katika moja ya fasiri za watʰu hawo wanaoishi upwa huwo huwo anawouzungumziya Tolmacheva na wengineo.

Hoja yetu ya kiisimu inashaḏiḏiya kuwa 'zanj' na 'shenzi' ni maneno mamoja isipokuwa mabaḏiliko yameṯokeya pengine kwa mpito wa wakaṯi, jambo ambalo hatulishughulikii katika makala haya, au ni ṯafauṯi za maṯamshi kulingana na waṯowaji na wapokezi wa neno hilo. Tukichukuliya kuwa asili ya neno lenyewe ni /shenzi/, /shinzi/, au /senzi/ (neno alilotumiya Sacleux uk. 602 kwamba laṯokana na lahaja mojawapo ya kiOmani [waArabu] na kiZaramo [waBantu]) basi tʰwaweza kusema kuwa kuliṯokeya mifanyiko ya kifonolojiya—udhoofikaji—uliyosababisha /sh/ kuwa /z/ kupitiya /s/. /sh/ ni sauṯi isoghuna iligeuka na kuwa /z/ ambayo ni ghuna (kuhusu mfanyiko huu rejeleya Katamba (1989, uk. 105)). Tʰwaweza kubashiri hivi:

/shenzi/>/senzi/>/zenzi/>/zengi/>/zenji/,/zangi/,/zanji/

/shinzi/>/sinzi/>/zinzi/>/zingi/>/zinji/

Neno walilonukuu waanḏishi wa kiArabu ni 'zanj' au 'zinj' na yaweza kuwa walilipata kuṯoka kwa waSwahili likiwa ni 'shenzi'/'shinzi', kumfuwata Krapf ambaye kamusi lake nrilo la zamani zaidi tulilorejeleya. Walakini, katika konsonanti za mwisho wa neno hilo ni ṯafauṯi

na walizorekodi waanḏishi. ‘zanj’, ‘zang’ ina fonimu /j/ na /g/ mṯawaliya tukiyonrowa nazali iliyomo. Kimaṯamshi waanḏishi walizisikiya sauṯi hizo na nriyo maana hawakuwacha kuziyanḏika. Ikiwa ni hivo basi, ni wazi kwamba asili ya neno shenzi lazima lilikuwa na /j, g/; tuseme asiliya yake lilikuwa /shengi, shenji, shangi, shanji/. Tolmacheva (1989 uk. 105) anasema kuwa neno ‘zanji’ lilianza kutumika katika maanḏiko ya kiArabu Karne ya 8. Tukumbuke piya kuwa neno hili lilirejeleya nchi iliyoko Afrika Mashariki; na fauka ya hayo, katika uṯafiṯi ulofanywa na Mark Horton katika mji wa Shanga (kikae humaanisha kusini na nriko uliko), Pate, Kenya mji huu ulikuwa na majumba yaliyojengwa katika Karne ya 8 (Wilson, 1999 uk. 191) hivo kutiliya nguvu makisiyo yetu kuwa ‘zanj’ ni ‘shang-a’ kwa sababu ya mfanyiko wa kifonolojiya wa udhoofikaji uloṯokeya katika neno hilo ikawa mwishowe laṯamkwa ‘shenzi’. Yaani, udhoofikaji umedhihiri katika konsonanti ya mwisho wa neno hilo /sha(e)ngi/, kuṯoka /g/ na kuwa /z/.

/shang-a/>/shanji/>/shanzi/, /shenzi/

Tuṯaona katika mfano huwo kuwa asili ni /shang/ ambapo /a/ ni kiishiyo cha neno na kwamba udhoofikaji ulisababisha /shanzi/. Mfanyiko wa aina hii umo katika kiSwahili ambapo kitenzi /jenga/ huwa /mjenzi/ kinapokuwa nomino. Piya, kuliṯokeya mageuko ya irabu ya kati /a/ kuwa /e/ kama katika neno /chafuwa, chefuwa/ au /kupawa, kupewa/ -- huu ni mpishano huru. Kwa hivo, kuṯokana na ufafanuzi wetu neno /shenzi/ asili yake ni /shanga/ na moja ya wanaṯi wake waitʰwa waNg’anru (Ahmad Sheikh Nabahany amesema ‘ng’anru kikaye ni dhahabu’ hivo kuvunja fikira za urangi weusi) ambawo nriyo mji wa azali katika mapisi ya waSwahili na nriyo waloukuta wasafiri na wafanyibiyashara waloṯembeleya sehemu hizi katika Karne ya 8 na kabla ulokuwa na ufanisi mkubwa haṯa wakaweza kuutaja katika maanḏiko yao.

**Nyoko**

Neno hili aghalabu kwa sasa matumizi yake yamebakiya katika maṯushi na huwa mwiko kuṯamkwa hadharani. Katika hali ya kutukanana watʰu husikika wakisema, ‘k*manyoko’ au katika msemo “alinyamaa kimya haṯa nyoko hakunambiya”. Sacleux (1939) na Taylor (1891) wameeleza kuwa ‘mama’ kizamani na kilahaja za kaskazini huitwa ‘inya’, ‘nyoko’, nina. Ajabu kwamba haṯa ‘nina’ katika kiSwahili cha kikawaida limehifadhiwa katika ṯushi ‘k*manina’.

**Usuli wa neno hili**

‘Nyoko’ ukitizama katika Kamusi nakalape ya TUKI wanafafanuwa kuwa ‘mama yako’. Katika lugha za kiBantu huṯamkwa ‘nyokwe’ kumaanisha ‘mama yako’. Kwa hivo, kiasiliya neno hili lina mofimu mbili zilizoshikana: ‘nyo’ na ‘ko’ /mama- + -ko/ ambayo imo katika tusi ‘k*mamako/k*ma mamako’. Lakini tukichunguza vizuri katika msemo tulotumiya hapo juu tuṯaona kuwa limetumika kama kihisishi ambacho chaṯokana na nomino. Pili, kulingana na Chum (1994), neno hili ‘nyoko’ piya limetumika mara mbili: 1) kama kihisishi chenye ‘athari ya kiutusi’ ambayo haiyonekani katika mfano anawouṯowa, ‘Nyoko, wenda upesi nkokutuma/Hebu nenda mara moja nilikokutuma’ kwa kiSanifu. 2) ‘Nyoko’ imerudiwa mara mbili kwa kushikanishwa: ‘Situkalie kinyokonyoko va/Usitukalie kiutomvu wa nidhamu hapa’ kiSanifu. Taylor na Sacleux wameitumiya nahau hii lakini kwa kuiweka kiumojaumoja: ‘Nyoko! Nyoko! ni shiba ya kuonana’ (Familiarity breeds contempt). Tuṯaona kuwa mifano yoṯʰe mitatu yataja ‘nyoko’ lakini haiyoneshi utusaji kama ilivojiṯokeza katika ‘k*manyoko’. Uwelezi wetu waoneleya kuwa yaonekana ‘nyoko’/mama yako’ ilipata athari ya uṯushi pinri iliposhikanishwa na ‘k*ma’ ‘the V-word’. Hii k*ma yenyewe piya si tusi bali yaṯokana na neno ‘kʰoma’ yenye maana ya ‘pango’. Mofimu hii ‘nyo’ piya inapatikana katika kihisishi ‘Nyoo!’ ambacho Taylor na Sacleux wamelitaja hilo. Lakini katika kihisishi hichi ina maana ya ‘kuonesha kuṯokubaliyana na jambo lizungumzwalo’.

Tukiyengezeya, katika matumizi ya kikawaida, ‘k*manyoko’, ‘k*manina’ hutumiwa waziwazi baina ya wasemaji kuonesha hasira au hata furaha (kimtaani husemwa, “k*manyoko Messi ulivoikata ngome nzima”) lakini si kumaanisha kutusiyana. Wazazi huweza kuiṯamka misemo hiyo bila ya kinyezi au haya kwa wazee wenzao au piya kwa watʰotʰo wao na wa wenzao. Tajriba nilonayo mimi tulipokuwa wadogo maneno haya si makosa kabisaa – tuliyatumiya bila ya ugomvi wowoṯʰe. Tusi baya kati ya yote ni ‘k*ma mamako/’k*mamako’. Hili ni mwiko na likitajwa baina ya wavutanao basi rabsha kubwa litatokeya. Nadhani ni kwa sababu wavutanao wanajuwa maana ya ‘mamako’ lakini, pengine, hawajuwi maana ya ‘nina’ au ‘nyoko’, au pengine, jamii yenyewe kwa kuṯojuwa kwao maana asiliya wamelitakasa kwamba ni sawa kutumiwa katika mukṯadha wa mvutano/mfarakano.

**Kuhiṯimisha**

Makala haya yaliyanza kwa kuchanganuwa maneno mawili ambayo kileo ni ‘matusi’ na huwa mwiko kuyatumiya hadharani au kwa mtʰu yoyoṯʰe. Shenzi na nyoko nriyo misamiyaṯi ya kiSwahili tuloishika kwa kwangaliya nyusuli zake kiisimu na kimatumizi ya kikawaida. Tumepata misamiyaṯi hino ina ufungamano na mapisi ya waSwahili na uṯamaduni wao. Lengo letu lilikuwa kuyatakasa maneno haya mawili kwa kujuza fasili zake ili watʰu wasiyone uzito katika kuyatumiya maongezini. Kuṯoka kuona huzuni kwa mtʰu kuitwa ‘mshenzi’ haḏi kufakhirika kuwa anasibishwa na kabila la watʰu wenyeji wa Afrika Mashariki. Badala ya kujibu, ‘mwenyewe’ (yaani “ukuregelee mwenyewe huwo ushenzi” kama tulivofunzwa udogoni kumjibu mtusaji) sasa tujibu ‘Hewaa!’ kuonesha uwafiki wa kusifiwa huko.

**Marejeleo**


Chimerah, R. (1995). *Nyongo mkalia ini*. Oxford University Press.

Chum, H. (1994). *Msamiati wa pekee wa Kikae: Kae specific vocabulary*. Nordic Association of African Studies.

Katamba, F. (1989). *An introduction to phonology*. Longman Group.

Krapf, L. (1882). *A dictionary of Suahili language*. Trubner & Co.

Sacleux, C. S. (1939). *Dictionnaire Swahili-Francais*. Institut d' Ethnologie.

Shaban, M. A. (1978). *Islamic history: A new interpretation*. Cambridge University Press.

Taylor, W. E. (1891). *African aphorisms*. Society for Promoting Christian Knowledge.

Tolmacheva, M. A. (1986). Towards a definition of the term Zanj. Imesomwa: https://www.jstor.org/stable/al.ch.document.sip200045

Wilson, T. H. (1999). Shanga: The archaeology of a muslim trading community on the coast of east Africa by Mark Horton: A review. Katika *The African Archaeological Review 16* (3), 191-195. Imesomwa: https://www.jstor.org/stable/25130678



**Kongole:** Wa kushukuriwa ni Mola kwa kutuwezesha kufanya juhuḏi zetu katika mwaka huu 2022; panapo majaaliwa Yake, tuṯaonana ṯena mwakani 2023.


**Dhamana:** Maelezo yaliyomo humu ni yangu na si ya UoK wala Iḏara yetʰu. Kwa loloṯʰe kuhusu makala haya, na Elimu kwa jumla, wasiliyana nami mkarama@kabianga.ac.ke .